TANZANIA PREMIER LEAGUE BOARD

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA

KAMATI ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) katika kikao chake cha Agosti 1, 2024 ilijadili na kufanyia maamuzi maoni ya maboresho ya Kanuni za Ligi kwa ajili ya toleo la 2024.

Kanuni zilizofanyiwa maboresho na kupitishwa katika kikao hicho ni pamoja na Kanuni ya 7 ya First League kuhusu Nane Bora na Kanuni 7 (saba) za Ligi Kuu ambazo ni Kanuni ya 9 kuhusu uwanja, Kanuni ya 17 kuhusu Taratibu za Mchezo, Kanuni ya 31 kuhusu Kutofika Uwanjani, Kanuni ya 47 kuhusu Udhibiti kwa Klabu, Kanuni ya 62 kuhusu Wachezaji wa Kigeni, Kanuni ya 77 kuhusu Makocha na Kanuni ya 79 kuhusu Maamuzi Yasiyokatiwa Rufaa.

Aidha kamati hiyo ilipitisha kanuni mpya 12 ambazo zitajumuishwa kwenye toleo la 2024.
Maboresho yote ya Kanuni za Ligi Kuu yaliyoainishwa kwenye jedwali hapa chini, yataathiri Kanuni za mashindano mengine yaliyo chini ya TFF na machapisho yake yatatangazwa.

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
7 Nane Bora (First League) **7:1**	Kutakuwa na Hatua ya Nane Bora (First League Top Eight) kwa Ligi Daraja la Pili itakayozikutanisha timu zilizoshika nafasi ya kwanza hadi ya nne (1-4) katika msimamo wa Ligi kwa kila kundi.	Timu vinara wa makundi baada ya kukamilika kwa michezo ya hatua ya makundi ya First League zitakuwa zimepanda daraja moja kwa moja kwenda Ligi ya Championship na timu zitakazoshika nafasi ya pili na ya tatu kwa kila kundi zitacheza michezo ya mtoano (play-off) ya kuwania kupanda daraja katika mfumo ufuatao; i. Timu katika nafasi ya pili kundi A itacheza dhidi ya timu katika nafasi ya tatu kundi B. ii. Timu katika nafasi ya pili kundi B itacheza dhidi ya timu katika nafasi ya tatu kundi A.
7:5	Timu zitakazoshindwa kufuzu katika hatua ya Nusu Fainali ya Nane bora zitabaki First League kwa msimu unaofuata.	
7:6	Timu Bingwa na timu itakayoshika nafasi ya Pili katika Hatua ya Nane bora zitapanda moja kwa moja kwenda Ligi Daraja la Kwanza (Championship).	

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
		iii. Washindi wa jumla katika michezo ya awali (i & ii), watacheza dhidi ya timu zilizoshindwa kwenye hatua ya mtoano ya kushuka daraja kwenye Ligi ya Championship kuwania nafasi mbili za kucheza Championship msimu unaofuata.
9 Uwanja	Timu ya Ligi Kuu inaweza kuteua viwanja vingine miongoni mwa viwanja visivyokuwa na michezo ya Ligi Kuu kwa michezo yake miwili tu ya nyumbani na kuwasilisha Uteuzi wake huo siku ishirini na moja (21) kabla ya mchezo husika inayokusudia kucheza kwenye uwanja wa uteuzi. Masharti ya uwasilishaji yatazingatia pia kanuni ya 9:3 ya Kanuni hizi. Uwanja ukishapitishwa hautabadilishwa isipokuwa kwa mazingatio ya Kanuni ya 9:6	Timu ya Ligi Kuu inaweza kuteua viwanja vingine miongoni mwa viwanja vilivyokaguliwa na kukidhi vigezo vya kikanuni kutumika kwa michezo ya Ligi Kuu kwa michezo yake miwili tu ya nyumbani na kuwasilisha Uteuzi wake huo siku ishirini na moja (21) kabla ya mchezo husika inayokusudia kucheza kwenye uwanja wa uteuzi. Masharti ya uwasilishaji yatazingatia pia kanuni ya 9:3 ya Kanuni hizi. Uwanja ukishapitishwa hautabadilishwa isipokuwa kwa mazingatio ya Kanuni ya 9:6
17:6 Taratibu za Mchezo	Timu zinazocheza mchezo husika zinatakiwa kuwasilisha kwa Kamishina/Mratibu (GC) wa mchezo Orodha ya Viongozi wasiozidi wanane (8) na wasiopungua watano (5) na Wachezaji wasiozidi ishirini (20) kwa mchezo husika masaa mawili kabla ya muda wa kuanza mchezo (kickoff). kwa kutumia fomu maalum iliyojazwa kwa unadhifu na ukamilifu ikiwa imesainiwa na kila mmoja.	6) Timu zinazocheza mchezo husika zinatakiwa kuwasilisha kwa Kamishina/Mratibu (GC) wa mchezo Orodha ya Viongozi wasiozidi tisa (9) na wasiopungua watano (5) kwa nafasi zilizoainishwa kwenye Kanuni ya 76:2 ya Ligi Kuu na wachezaji wasiozidi ishirini na mmoja (21) kwa mchezo husika masaa matatu (3) kabla ya muda wa kuanza mchezo (kickoff) kwa kutumia fomu maalum iliyojazwa kwa unadhifu na ukamilifu.

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
		i. Fomu maalum ni lazima iwe na mfumo (formation) wa uchezaji. ii. Fomu maalum ni lazima iwe imesainiwa na kila mmoja. iii. Klabu ya Ligi Kuu inawajibika kujumuisha wachezaji wasiopungua wawili (2) kutoka katika timu zake za vijana kwenye orodha ya wachezaji 21 kwa ajili ya kila mchezo wa Ligi Kuu.
17:7 Taratibu za Mchezo	Kila klabu ya Ligi Kuu ina wajibu wa kuhakikisha linakuwepo Gari la wagonjwa (ambulance) na vijana waokota mipira (ball kids) uwanjani katika kila mchezo wake wa nyumbani timu yake inapocheza. Iwapo huduma hizo hazitakuwepo, Kamishna atazuia mchezo kuchezwa, na timu mwenyeji itapoteza mchezo huo.	Kila klabu ya Ligi Kuu ina wajibu wa kuhakikisha linakuwepo Gari la wagonjwa (ambulance), watoa huduma ya kwanza, walinzi wa uwanjani (stewards) na vijana waokota mipira (ball kids) uwanjani katika kila mchezo wake wa nyumbani timu yake inapocheza. Iwapo huduma hizo hazitakuwepo, Kamishna atazuia mchezo kuchezwa, na timu mwenyeji itapoteza mchezo huo. i. Klabu itawajibika na kuadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi kwa vitendo vyovyote visivyo vya kiuanamichezo au vinavyovunja taratibu za mchezo vitakavyofanywa na watoa huduma ya kwanza, walinzi wa uwanjani (stewards), watoto waokota mipira

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
		(ball kids) na watoa huduma wengine wanaoletwa na klabu.
17:15 Taratibu za Mchezo	Timu zinatakiwa kufika uwanjani si chini ya dakika 90 (tisini) kabla ya muda wa kuanza mchezo.	Timu zinatakiwa kufika uwanjani si chini ya dakika 90 (tisini) kabla ya muda wa kuanza mchezo na kulazimika kufuata ratiba ya matukio ya mchezo (count down) kama itakavyotolewa na mratibu wa mchezo. i. Baada ya kuwasili uwanjani katika muda wa kikanuni, wachezaji na maofisa wa benchi la ufundi wa timu wanaruhusiwa kuzuru kiwanja kwa muda usiozidi dakika kumi (10).
17:60 Taratibu za Mchezo	TFF/TPLB itachukua hatua kwa ukiukwaji wowote wa Taratibu za Mchezo kama zilivyoainishwa kwenye kanuni ya 17 kwa kutoa Onyo kali au karipio au kutoza faini kuanzia shilingi laki tano (500,000/-) mpaka shilingi milioni moja (1,000,000/-) na/au kufungia michezo isiyozidi mitatu (3) au kipindi kisichozidi miezi mitatu (3). Faini kwa makosa yanayojirudia itatozwa kati ya shilingi milioni moja (1,000,000/-) na shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa mchezaji, kiongozi au timu.	TFF/TPLB itachukua hatua kwa ukiukwaji wowote wa Taratibu za Mchezo kama zilivyoainishwa kwenye kanuni ya 17 kwa kutoa Onyo kali au karipio au kutoza faini kuanzia shilingi milioni moja (1,000,000/-) mpaka shilingi milioni mbili (2,000,000/-) na/au kufungia michezo isiyozidi mitatu (3) au kipindi kisichozidi miezi mitatu (3). Faini kwa makosa yanayojirudia itatozwa kati ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) na shilingi milioni kumi (10,000,000/-) kwa mchezaji, kiongozi au timu.
31:1(1.3) Kutofika Uwanjani	Timu yoyote itakayokosa kufika uwanjani bila ya sababu za msingi zinazokubalika kwa TFF/TPLB na/au kusababisha mchezo	Timu yoyote itakayokosa kufika uwanjani bila ya sababu za msingi zinazokubalika kwa TFF/TPLB na/au kusababisha mchezo

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
	usifanyike itakabiliwa na adhabu zifuatazo: 1.1 Kutozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) ambapo shilingi milioni mbili na laki tano (2,500,000/-) itachukuliwa na Bodi ya Ligi Kuu na shilingi milioni mbili laki tano (2,500,000/-) italipwa kwa timu pinzani. 1.2 Kulipa fidia ya maandalizi/uharibifu wowote unaoweza kujitokeza. 1.3 Kupokwa alama 15 (kumi na tano) katika msimamo wa Ligi na viongozi waliosababisha jambo hilo watachukuliwa hatua zaidi za kinidhamu. 1.3.1 Endapo timu itakuwa na alama pungufu ya 15, itakuwa na alama hasi kwa kiasi kinachopungua kwenye msimamo wa Ligi. 1.3.2 Endapo timu itamaliza msimu wa Ligi ikiwa na alama	usifanyike itakabiliwa na adhabu zifuatazo: 1.1 Kutozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) ambapo shilingi milioni mbili na laki tano (2,500,000/-) itachukuliwa na Bodi ya Ligi Kuu na shilingi milioni mbili laki tano (2,500,000/-) italipwa kwa timu pinzani. 1.2 Kulipa fidia ya maandalizi/uharibifu wowote unaoweza kujitokeza. 1.3 Kupokwa alama 15 (kumi na tano) katika msimamo wa Ligi na viongozi waliosababisha jambo hilo watachukuliwa hatua zaidi za kinidhamu. 1.3.1 Endapo timu itakuwa na alama pungufu ya 15, itakuwa na alama hasi kwa kiasi kinachopungua kwenye msimamo wa Ligi. 1.3.2 Endapo timu itamaliza msimu wa Ligi

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
	hasi, itaanza na alama hizo hasi katika msimamo wa Ligi kwenye msimu unaofuata wa Ligi ya hadhi yake.	ikiwa na alama hasi, itaanza na alama hizo hasi katika msimamo wa Ligi kwenye msimu unaofuata wa Ligi ya hadhi yake.
	1.4 Itapoteza haki ya kuchukua gawio lake la mapato ya mchezo huo.	1.4 Kwa michezo ya hatua ya mtoano, timu iliyokosa kufika uwanjani itakuwa imepoteza hadhi ya kuingia hatua inayofuata bila kujali matokeo ya mchezo uliochezwa.
	1.5 Kiongozi yeyote atakayebainika kushiriki, alishawishi au alikuwa chanzo au sababu ya timu kutotokea uwanjani bila ya sababu za msingi atafungiwa kwa kipindi cha miezi kumi na miwili (12).	1.5 Itapoteza haki ya kuchukua gawio lake la mapato ya mchezo huo.
	1.6 Inaweza kukabiliwa na adhabu zaidi kama ambavyo TFF/TPLB itahitaji kuchukua hatua zaidi kadiri itavyoona inafaa.	1.6 Kiongozi yeyote atakayebainika kushiriki, alishawishi au alikuwa chanzo au sababu ya timu kutotokea uwanjani bila ya sababu za msingi atafungiwa kwa kipindi cha miezi kumi na miwili (12).
	1.7 Timu yoyote iliyopewa adhabu ya faini chini ya kanuni 31:1(1.1, 1.2 na 1.3) haitaruhusiwa kucheza hadi itakapotekeleza adhabu hiyo kwa daraja ambalo itakuwa ipo.	1.7 Inaweza kukabiliwa na adhabu zaidi kama ambavyo TFF/TPLB itahitaji kuchukua hatua zaidi kadiri itavyoona inafaa.

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
		1.8 Timu yoyote iliyopewa adhabu ya faini chini ya kanuni 31:1(1.1, 1.2 na 1.3) haitaruhusiwa kucheza hadi itakapotekeleza adhabu hiyo kwa daraja ambalo itakuwa ipo.
47:1 Udhibiti kwa Klabu	Klabu ina wajibu na jukumu la kuhakikisha kuwa wachezaji, viongozi, wanachama na wapenzi wake wanajiheshimu na hawajihusishi na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu kama vile matusi, vitisho, vurugu, vitendo vinavyoashiria imani za kishirikina na vitendo vyovyote vingine visivyokuwa vya kimichezo kwenye viwanja vya michezo. Klabu ambayo mashabiki/wachezaji/viongozi wake watafanya vitendo hivyo itatozwa faini ya shilingi Milioni moja (1,000,000/-).	Klabu ina wajibu na jukumu la kuhakikisha kuwa wachezaji, viongozi, wanachama na wapenzi wake wanajiheshimu na hawajihusishi na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu kama vile matusi, vitisho, vurugu, vitendo vinavyoashiria imani za kishirikina na vitendo vyovyote vingine visivyokuwa vya kimichezo kwenye viwanja vya michezo. Klabu ambayo mashabiki/wachezaji/viongozi wake watafanya vitendo hivyo itatozwa faini ya shilingi Milioni tano (5,000,000/-). i. Kwa makosa ya kujirudia, faini itatozwa kati ya shilingi milioni kumi (10,000,000) na milioni ishirini (20,000,000).
62:5 Wachezaji wa Kigeni	Mchezaji yeyote wa kigeni anayesajiliwa katika Ligi Kuu atalipiwa ada maalum ya shilingi milioni nne (4,000,000/-) kwa msimu ili usajili wake uweze kuthibitishwa na kuruhusiwa kucheza.	Mchezaji yeyote wa kigeni anayesajiliwa katika Ligi Kuu atalipiwa ada maalum ya Sh. 8,000,000 (milioni nane) kwa msimu ili usajili wake uweze kuthibitishwa na kuruhusiwa kucheza.

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
77:5 Makocha	Kocha Msaidizi na kocha wa timu ya vijana (U20 na U17) wa klabu ya Ligi Kuu awe na Leseni ya chini kuanzia Daraja C ya CAF au inayolingana nayo iliyotolewa na Mashirikisho ya Mabara mengine yanayotambuliwana FIFA.	Kocha Msaidizi na kocha wa timu ya vijana (U20 na U17) wa klabu ya Ligi Kuu awe na Leseni ya chini kuanzia B Diploma ya CAF au inayolingana nayo iliyotolewa na Mashirikisho ya Mabara mengine yanayotambuliwana FIFA. Kocha msaidizi wa timu ya vijana (U20 na U17) kutoka nje ya bara la Afrika anatakiwa kuwa na angalau A Diploma au inayolingana nayo.
77:6 Makocha	Klabu ya Ligi Kuu inawajibika kuwa na kocha wa walinda mlango (goalkeepers) mwenye ujuzi, klabu itakayokosa kocha wa walinda mlango itakabiliwa na adhabu kwa mujibu wa kanuni hizi.	Klabu ya Ligi Kuu inawajibika kuwa na kocha wa walinda mlango (goalkeepers) na kocha wa viungo (Fitness Coach) wenye ujuzi, klabu itakayokosa kocha wa walinda mlango na kocha wa viungo itakabiliwa na adhabu kwa mujibu wa kanuni hizi.
	(1) Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayoanza msimu mpya na kucheza mchezo wa Ligi bila kuwa na daktari mwenye ujuzi kwa kanuni ya 78:1 itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na daktari anayehitajika, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja. (i) Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayopoteza daktari mwenye ujuzi kwa kanuni ya 78:1 baada ya kuanza msimu itaruhusiwa kutumia daktari wa muda	(2) Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayoanza msimu mpya na kucheza mchezo wa Ligi bila kuwa na daktari mwenye ujuzi kwa kanuni ya 78:1 au/na mtaalam wa tiba ya viungo itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na daktari anayehitajika, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja. (iii) Timu yoyote ya Ligi Kuu itakayopoteza daktari mwenye ujuzi kwa kanuni ya 78:1 au/na mtaalam wa tiba ya viungo baada ya kuanza

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI	ILIVYOKUWA AWALI	ILIVYO SASA
	mwenye sifa za kuwa daktari msaidizi kwa mujibu wa kanuni, kwa michezo isiyozidi sita (6) ya Ligi Kuu. (ii) Kama itakuwa haijapata daktari mkuu mwenye ujuzi hadi baada ya michezo hiyo sita (6), itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na daktari anayehitajika kikanuni, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja.	msimu itaruhusiwa kutumia wataalam wa muda wenye sifa za kuwa daktari msaidizi kwa mujibu wa kanuni au/na mtaalam wa tiba ya viungo msaidizi, kwa michezo isiyozidi sita (6) ya Ligi Kuu. (iv) Kama itakuwa haijapata daktari mkuu au mtaalam wa tiba ya viungo mwenye ujuzi hadi baada ya michezo hiyo sita (6), itatozwa faini ya shilingi milioni tano (5,000,000/-) kwa kila mchezo kwa michezo mpaka sita (6) ya Ligi Kuu, endapo bado itashindwa kutimiza sharti hili la kuwa na daktari na/au mataalam wa tiba viungo anayehitajika kikanuni, itaondolewa kwenye Ligi Kuu na kushushwa daraja.
79 Maamuzi yasiyokatiwa rufaa	Maamuzi yote kwa mujibu wa vipengele vya kanuni za Ligi Kuu katika kanuni ya 79 hayatakatiwa rufaa katika ngazi yoyote, mhusika yeyote kuhusiana na maamuzi yaliyotolewa chini ya vipengele hivi anawajibika kutekeleza linalomhusu mara moja.	Vipengele vya kanuni kwa makosa yanayoweza kukatiwa rufaa (kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 79) viondolewe adhabu na badala yake vielekeze kuwa mhusika atafikishwa kwenye Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili ya TFF.

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

KANUNI MPYA	
SURA YA III **Ligi** 1).	Katika kuongeza uwajibikaji na hamasa kwa klabu wakati wa maandalizi ya michezo ya Ligi, klabu zimepewa mamlaka ya kusimamia shughuli zote za maandalizi ya mchezo ukiwemo mchakato wa kuuza tiketi kwa njia ya Elektroniki. Muongozo wa uuzaji tiketi utatolewa na TFF/TPLB. i. Mamlaka ya kuandaa na kusimamia ugawaji wa vitambulisho vya msimu pamoja na mialiko ya watu maalum (VVIP) na jukwaa la watu maalum, yatakuwa chini ya TFF na TPLB.
2).	Kila klabu italazimika kuteua na kuitangaza angalau siku moja katika kila mwezi, ambayo itakuwa maalum kwa ajili ya wanahabari kufanya mahojiano na wachezaji, maafisa wa ufundi na viongozi wa klabu kwa lengo la kuitangaza timu na Ligi kwa ujumla.
3).	Kutakuwa na siku maalum ya mdhamini mwenye haki ya matangazo ya runinga kutangaza matukio ya timu moja ya Ligi Kuu kuanzia maandalizi ya mwisho ya mchezo (mazoezi), chakula cha mchana, kuwasili uwanjani pamoja na baadhi ya matukio ya chumba cha kuvalia.
4).	Timu ya Ligi Kuu inawajibika kuutangaza kila mchezo wa nyumbani wa Ligi kwa kutumia njia mbalimbali na kuhakikisha kunakuwa na mfumo wa sauti uwanjani kwa ajili kutoa burudani na matangazo kwa mashabiki.

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz **CEO:** Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

5). **77: Makocha**	Kocha mkuu wa klabu ya Ligi Kuu kutoka nje ya bara la Afrika anatakiwa kuwa na angalau Pro Diploma. Kocha msaidizi wa klabu ya Ligi Kuu kutoka nje ya bara la Afrika anatakiwa kuwa na angalau A Diploma au inayofanana nayo.
6).	Kocha wa timu ya Ligi Kuu kutoka nje ya Tanzania ni lazima awe amefundisha klabu ya Ligi Kuu au timu ya Taifa katika nchi yoyote au ndani ya kipindi cha miaka miwili iliyopita.
7). **31: Kutofika uwanjani**	31:1(1.8) Timu itakayoshindwa kufika kituoni katika michezo mitatu (3) ya Ligi bila sababu za msingi zinazokubalika na TFF/TPLB itakuwa imejiondoa kushiriki Ligi hiyo.
8). **7: Michezo ya Mchujo**	7:8 Katika michezo ya mchujo, timu iliyomchezesha mchezaji aliyethibitishwa usajili wake lakini aliyebainika kubadili jina kwa nia ya kudanganya au kubainika kutumika udanganyifu mwingine wowote kufanikisha kukamilisha usajili wake au mchezaji aliyebainika usajili wake kuwa na kasoro baada ya kuthibitishwa italipa faini kati ya shilingi milioni (1,000,000/-) na shilingi milioni tano (5,000,000/-) na itakuwa imepoteza mchezo huo na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata, timu pinzani itapewa alama tatu na mabao matatu pamoja na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata bila kujali matokeo ya mchezo mwingine uliochezwa. 7:9 Katika michezo ya mchujo timu itakayobainika kumchezesha mchezaji ambaye hajasajiliwa itapoteza mchezo husika, italipa faini ya shilingi milioni mbili (2,000,000/-) na mchezaji husika atafungiwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili (12) bila ya kujali kulalamikiwa au la, itakuwa imepoteza mchezo huo na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata, timu pinzani itapewa alama tatu na mabao matatu pamoja na hadhi ya kuendelea hatua inayofuata bila kujali matokeo mchezo mwingine uliochezwa.
9).	Kutakuwa na shindano la Kombe la Muungano ambalo litahusisha timu mbili kutoka Tanzania Visiwani na mbili kutoka Tanzania Bara.

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3

P.O. Box 79043, Tel 222850997, Fax 222850997
Email: info@ligikuu.co.tz Web: www.ligikuu.co.tz
14th Floor, NSSF Mafao House Plot No. 40, Block Y
Uhuru Street - Ilala, Dar es Salaam

10).	Michezo ya Ligi inaweza kuchezwa kwenye viwanja vilivyopo Tanzania visiwani (Zanzibar) kwa mazingatio ya Kanuni 9 kuhusu Uwanja.
11). **Kanuni ya 47:33 - Udhibiti kwa Klabu**	Timu ya Ligi Kuu itakayoshindwa kufuata na kutekeleza masharti yote yaliyoainishwa kwenye Kanuni ya Leseni za Klabu, itaadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi
12). **Kanuni ya 40:6 - Udhibiti Kimashindano**	Ni marufuku kwa kocha, mchezaji, kiongozi au ofisa wa mchezo kushiriki michezo ya kubashiri (betting). Kocha, mchezaji, kiongozi au ofisa wa mchezo atakayekiuka, atafungiwa maisha kujihusisha na mpira wa miguu.

Imetolewa na;

Idara ya Habari na Mawasiliano
Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB)
Agosti 7, 2024

Chairman: Steven J. Mnguto Email: s.mnguto@ligikuu.co.tz CEO: Almasi J. Kasongo Email: a.kasongo@ligikuu.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe. azamtv TBC UKWELI NA UHAKIKA TV3